



REALISING SUSTAINABLE
DEVELOPMENT GOALS IN AFRICA:
PROGRESS AND WAY FORWARD

7 - 8 April 2025 | Kampala, Uganda

Tangazo kwa Vyombo vya Habari

MWALIKO KWA VYOMBO VYA HABARI

Nini: Taasisi ya UONGOZI inaandaa Kongamano la 8 la Kikanda la Viongozi wa Afrika (*African Leadership Forum*) lenye mada “*Kutimiza malengo ya maendeleo endelevu Afrika: Hatua zilizotekelezwa na mwelekeo wa baadaye*”. Kongamano hili ni tukio muhimu litakalofanyika kabla ya Mkutano wa 11 wa Kikanda wa Maendeleo Endelevu wa tarehe 9 – 11 Aprili 2025, unaoratibiwa na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Uchumi Barani Afrika (UNECA).

Nani: Kongamano la 8 la Kikanda la Viongozi wa Afrika linaitishwa na **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Mlezi wa Kongamano na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na **Mhe. Hailemariam Dessalegn Boshe**, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia.

Lini: 7 – 8 Aprili 2025.

Wapi: Speke Resort Munyonyo, Kampala, Uganda.

Namna: Kongamano litajumuisha ufunguzi na mijadala itakayojikita kwenye mada kuu nne:

- i. Kutokomeza umaskini na kukuza uchumi;
- ii. Afya bora na ustawi;
- iii. Kuimarisha elimu na ujuzi; na
- iv. Mifumo madhubuti na endelevu ya kusimamia mazingira.

Lengo: Kongamano hili linalenga kutoa fursa ya kujadili hatua zilizofikiwa katika utekelezaji, changamoto, na namna ya kuyafikia malengo ya maendeleo endelevu barani Afrika. Malengo mahususi ni:

- i. Kujadili hatua zilizofikiwa na nchi za Afrika katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu;
- ii. Kuainisha changamoto zinazokwamisha utekelezaji;
- iii. Kutengeneza mipango inayotekelezeka kwa ajili ya kutatua changamoto katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu;
- iv. Kuhamasisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu baina ya nchi za Afrika; na



REALISING SUSTAINABLE
DEVELOPMENT GOALS IN AFRICA:
PROGRESS AND WAY FORWARD

7 - 8 April 2025 | Kampala, Uganda

- v. Kuleta mbinu zenye ubunifu na kuimarisha mashirikiano kwa ajili ya kuchochea maendeleo endelevu.

Mgeni rasmi: Mhe. Gen Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda.

Washiriki: Washiriki wa Kongamano ni pamoja na Mhe. Dkt. Mohamed Moncef Marzouki, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Tunisia; na Mhe. Dkt. Ernest Bai Koroma, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Sierra Leone.

Washiriki wengine ni viongozi waandamizi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika – na sekta zote ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, sekta ya elimu ya juu, na sekta ya asasi za kiraia.

Waandishi wa habari wanaalikwa kwa ajili ya kuhudhuria tukio la ufunguzi tarehe 7 Aprili 2025 kuanzia saa 2:00 Asubuhi – 7:00 Mchana, na tukio la kufunga tarehe 8 Aprili 2025 kuanzia 7:00 Mchana – 7:45 Mchana ambapo muhtasari wa Kongamano utawasilishwa.

Kuhusu Taasisi ya UONGOZI: Taasisi ya Uongozi kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu Barani Afrika, maarufu kama Taasisi ya UONGOZI (*UONGOZI Institute*), ni taasisi ya kikanda ya kuimarisha kada ya uongozi iliyo chini ya Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taasisi ilianzishwa mwaka 2010 na Serikali za Tanzania na Finland kwa lengo la ya kujenga na kuimarisha viongozi wa Afrika ili kukidhi matakwa ya ndani ya kutoa huduma kwa wananchi na kuyafikia maendeleo endelevu.

Taasisi inatambua kwamba sifa za uongozi hujengwa kwa namna endelevu. Hivyo, programu katika mihimili yake miwili – uongozi na maendeleo endelevu – zinatekelezwa kupitia maeneo makuu manne: mafunzo ya uongozi, mijadala ya kisera, tafiti, na ushauri wa kitaalamu. Wateja wake ni pamoja na taasisi na watu binafsi kutoka kwenye sekta zote.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na: Suzana Aroko, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mahusiano kwa Umma, Taasisi ya UONGOZI | Barua pepe: saroko@uongozi.or.tz | www.uongozi.go.tz

Shiriki katika mjadala mtandaoni: #ALF2025 #ARFSD11